JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

MWONGOZO WA

UTEUZI WA VIONGOZI WA ELIMU KATIKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA NA MIKOA

Julai, 2022

Umeandaliwa na

Ofisi ya Rais - TAMISEMI,
S. L P 1923, DODOMA

NENO LA WAZIRI

Waziri wa Nchi - OR TAMISEMI,
Mhe. Innocent L. Bashungwa (Mb)

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea na juhudi za kuboresha utoaji wa elimu nchini kwa kutoa fedha za ujenzi wa vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo na mabweni katika Shule za Sekondari na Vituo Shikizi vya Shule. Aidha, Rais, amekuwa akitoa maelekezo ya kuboresha utoaji wa elimu nchini sawa na Matamko ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka, 2014. Hivyo, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa ninampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake za kuwezesha upatikanaji wa elimu bora ya Msingi na Sekondari.

Kwa ajili ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka, 2014 hususan tamko namba 3.5.2 ambalo linaeleza kuwa, Serikali itaweka utaratibu wa kuteua na kutambua nafasi za usimamizi wa utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo katika ngazi ya Mkoa, Halmashauri, Kata na Shule ili ziwe na hadhi maalumu katika utumishi.

Katika kutekeleza hayo, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeandaa Mwongozo wa Uteuzi wa Viongozi wa Elimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mikoa.

Mwisho, ninaelekeza watendaji katika ngazi zote kusimamia utekelezaji wa mwongozo huu.

Innocent L. Bashungwa, (Mb)
WAZIRI WA NCHI

Dibaji

Katibu Mkuu - OR TAMISEMI,
Prof. Riziki S. Shemdoe

Utoaji wa Elimu Bora pamoja na mambo mengine, hutegemea uwepo wa viongozi bora wanaosimamia utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo. Hivyo, uteuzi wa Viongozi wa Elimu unapaswa kufanywa kwa kuzingatia mambo mbalimbali yakiwemo weledi, uadilifu na uzoefu katika kuongoza watendaji wa elimu. Kwa sababu hiyo, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imeandaa Mwongozo huu kwa lengo la kuweka bayana taratibu zinazopaswa kuzingatiwa katika uteuzi wa viongozi wa elimu katika ngazi za Shule, Kata, Halmashauri na Mikoa ili kuboresha usimamizi wa utoaji wa Elimu nchini.

Mwongozo huu umebainisha, pamoja na mambo mengine, nafasi za uongozi katika ngazi za Shule, Kata, Halmashauri na Mikoa. Aidha, sifa za kimuundo na kiutendaji zimewekwa bayana ikiwa ni pamoja na kuonesha Muundo wa Kamati za Mapendekezo ya Uteuzi zitakavyofanya uchambuzi na kuwasilisha mapendekezo yake kwa Mamlaka za Uteuzi. Aidha, Mwongozo umetoa maelezo fasaha ya kuzingatiwa na mamlaka za uteuzi zinapopitia mapendekezo ya Kamati wakati wa kuwateua wahusika kushika nyadhifa za uongozi wa elimu katika ngazi husika.

Mwongozo huu utatumiwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.
Ni matumaini yangu kuwa utekelezaji wa mwongozo huu utasaidia kuboresha usimamizi na uendeshaji wa Elimumsingi na Sekondari.

Prof. Riziki S. Shemdoe
KATIBU MKUU

Shukurani

Naibu Katibu Mkuu (E) - OR TAMISEMI,
Dkt. Charles E. Msonde

Mwongozo wa Uteuzi wa Viongozi wa Elimu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mikoa umeandaliwa kwa kuhusisha wataalamu kutoka Ofisi ya Rais -TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ninatoa shukrani za pekee kwa mwenyekiti, Bw. Ernest X. Hinju (Katibu Tawala Msaidizi Elimu - Mbeya) na wajumbe wake Bw. Abel A. Ntupwa (Katibu Tawala Msaidizi Elimu - Arusha), Bw. Riaz Abeid (Afisa Ofisi ya Rais – TAMISEMI), Bi. Theresia P. Kuiwite (Afisa Ofisi ya Rais – TAMISEMI) na Bw Noel F. Mafumiko (Afisa Ofisi ya Rais – TAMISEMI).

Aidha, ninawashukuru pia Wakurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Elimu Bw. Ephraim Simbeye (Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Elimu), Bi. Suzana Nussu (Mkurugenzi Msaidizi Elimu ya Awali na Msingi), Bi. Hadija Mcheka (Mkurugenzi Msaidizi Sekondari) na Bw. Geni Migeha (Mkurugenzi Msaidizi Elimu Maalum, Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi) kwa kuratibu zoezi hilo.

Ni matarajio ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI na wadau wa elimu kuwa, utekelezaji wa mwongozo huu utaisaidia Serikali kuongeza ufanisi katika usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini.

Dkt. Charles E. Msonde
Naibu Katibu Mkuu (Elimu)

Vifupisho vya Maneno

Ofisi ya Rais – MUUUB	Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora
Ofisi ya Rais – TAMISEMI	Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
MSM	Mamlaka za Serikali za Mitaa
WyEST	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia
TSC	Teachers' Service Commission

Yaliyomo

Dibaji i
Shukurani ii
Vifupisho vya Maneno iii

SURA YA KWANZA
MAMLAKA YA UTEUZI WA VIONGOZI WA ELIMU KATIKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA NA MIKOA 1
1.1 Utangulizi 1
1.2 Usuli 1
1.3 Umuhimu wa Mwongozo 2
1.4 Malengo ya Mwongozo 2
1.5 Matarajio 2
1.6 Hitimisho 2

SURA YA PILI
SIFA ZA VIONGOZI WA ELIMU KATIKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA NA MIKOA 3
2.1 Utangulizi 3
2.2 Mwalimu Mkuu 3
2.3 Mkuu wa Shule 4
2.4 Afisaelimu Kata 4
2.5 Afisaelimu Taaluma Msingi/Sekondari wa Halmashauri 5
2.6 Afisaelimu Vifaa na Takwimu Msingi / Sekondari wa Halmashauri 6
2.7 Afisaelimu wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi wa Halmashauri 6
2.8 Afisaelimu Elimu Maalum wa Halmashauri 7
2.9 Afisaelimu wa Halmashauri Msingi/Sekondari 8
2.10 Afisaelimu Taaluma Mkoa 9
2.11 Afisaelimu wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi Mkoa 9
2.12 Afisaelimu wa Mkoa 10
2.13 Hitimisho 11

SURA YA TATU
UTARATIBU WA UTEUZI WA VIONGOZI WA ELIMU KATIKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA NA MIKOA 12
3.1 Utangulizi 12
3.2 Uteuzi wa Mwalimu Mkuu 12
3.2.1 Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi 12

3.2.2 Mchakato wa Mapendekezo ya Uteuzi 13
3.2.3 Mamlaka ya Uteuzi 13
3.3 Uteuzi wa Mkuu wa Shule 14
3.3.1 Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi 14
3.3.2 Mchakato wa Mapendekezo ya Uteuzi 14
3.3.3 Mamlaka ya Uteuzi 14
3.4 Uteuzi wa Afisa Elimu Kata 14
3.4.1 Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi 14
3.4.2 Mchakato wa Mapendekezo ya Uteuzi 15
3.4.3 Mamlaka ya Uteuzi 15
3.5 Uteuzi wa Afisaelimu Msingi/Sekondari wa Halmashuri 16
3.5.1 Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi 16
3.5.2 Mchakato wa Mapendekezo ya Uteuzi 16
3.5.3 Mamlaka ya Uteuzi 16
3.6 Uteuzi wa Afisaelimu Taaluma, Afisaelimu Vifaa na Takwimu, Afisaelimu Elimu Maalumu na Afisaelimu Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi wa Halmashauri 17
3.6.1 Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi 17
3.6.2 Mchakato wa Mapendekezo 17
3.6.3 Mamlaka ya Uteuzi 17
3.7 Uteuzi wa Afisaelimu Taaluma Mkoa/Afisaelimu Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi wa Mkoa 18
3.7.1 Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi 18
3.7.2 Mchakato wa Mapendekezo ya Uteuzi 18
3.7.3 Mamlaka ya Uteuzi 19
3.8 Uteuzi wa Afisaelimu wa Mkoa 19
3.8.1 Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi 19
3.8.2 Mchakato wa Mapendekezo ya Uteuzi 19
3.8.3 Mamlaka ya Uteuzi 20
3.9 Utaratibu wa Kutengua Viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mikoa
3.10 Hitimisho 20

SURA YA NNE

KANUNI ZA UENDESHAJI WA KAMATI ZA MAPENDEKEZO YA UTEUZI WA VIONGOZI WA ELIMU KATIKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA NA MIKOA ... 15
4.1 Utangulizi 21
4.2 Kanuni za Uendeshaji wa Kamati za Uteuzi 21

SURA YA TANO

MAJUMUISHO NA HITIMISHO 22
5.1 Utangulizi 22
5.2 Majumuisho 22
5.3 Hitimisho 22

SURA YA KWANZA

MAMLAKA YA UTEUZI WA VIONGOZI WA ELIMU KATIKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA NA MIKOA

1.1 Utangulizi

Sura hii ina vipengele vitano (05) ambavyo ni usuli, umuhimu wa mwongozo, malengo ya mwongozo, matarajio na hitimisho.

1.2 Usuli

Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Ofisi ya Rais – TAMISEMI) ina jukumu la kusimamia na kuendesha Shule za Msingi na Sekondari kupitia Sheria za Serikali za Mitaa Na. 7, 8 na 9 za mwaka 1982 na kurekebishwa mwaka 2000 ambapo zinatoa maagizo ya usimamizi na uendeshaji wa Elimu ya Awali na Msingi kuwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, tamko la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kugatua Usimamizi na Uendeshaji wa Shule za Sekondari la tarehe 12 Februari, 2008 wakati wa Uteuzi wa Baraza Jipya la Mawaziri lilihamisha uendeshaji na usimamizi wa Shule za Sekondari kutoka Wizara ya Elimu kwenda TAMISEMI. Hivyo, ni jukumu la OR-TAMISEMI kubainisha na kusimamia miongozo ya uteuzi wa viongozi wa elimu katika ngazi za Shule, Kata, Halmashauri na Mikoa.

Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka, 1978 imetaja kwa ujumla utaratibu wa uteuzi wa viongozi wa Elimu. Sheria hiyo imefafanuliwa kupitia Kanuni za Elimu za mwaka, 2002 (*The Education Procedure and Qualifications of Appointment to Education Posts Regulations*) ambazo zinasisitiza kuwa uteuzi wa viongozi wa elimu kufanywa kupitia Kamati Maalum ambazo zitaundwa kuchambua na kufanya mapendekezo kwa Mamlaka ya Uteuzi kabla ya kujaza nafasi ya uongozi katika elimu.

Uteuzi wa viongozi katika Elimu hufanyika ili kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa mitaala na hatimaye kuboresha utoaji wa elimu nchini. Viongozi wa Elimu ni nguzo muhimu katika kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji. Hivyo, uteuzi wa viongozi wa elimu hupaswa kufanywa kwa umakini kabla ya kuwakabidhi dhamana ya kuongoza. Katika muktadha huo, Serikali itaendelea kufanya uteuzi wa viongozi wa elimu kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekretarieti za Mikoa ambapo utendaji kazi unaonekana kulegalega au kwa lengo la kuziba nafasi ambazo huachwa wazi na viongozi ambao walikuwa wanahudumu kutokana na kukoma utumishi wa

umma, kifo, kuondolewa katika nafasi au kujiuzulu.

1.3 Umuhimu wa Mwongozo

Mwongozo huu umelenga kuweka bayana taratibu za uteuzi wa viongozi wa Elimumsingi na Sekondari katika ngazi zote ili kupata viongozi bora. Aidha, mwongozo utarahisisha utendaji kazi kwa kuwa umekusanya pamoja maelekezo yaliyopo katika sheria, kanuni na nyaraka zinazohusiana na uteuzi zilizotolewa na mamlaka mbalimbali kwa urahisi wa utekelezaji.

Uchambuzi wa hali ya utekelezaji wa maelekezo ya uteuzi wa viongozi kwenye eneo la Elimumsingi na Sekondari umebaini kuwa maelekezo ya uteuzi wa viongozi yametawanyika hivyo kuleta changamoto kwa viongozi wakati wa utekelezaji. Hali hiyo, husabisha baadhi ya viongozi ambao wanateuliwa kuwa na ufanisi hafifu na wengine kushindwa kuthibitishwa kwa kuwa wanateuliwa kinyume na sifa na maelekezo ya uteuzi yaliyopo.

1.4 Malengo ya Mwongozo

Lengo kuu la mwongozo huu ni kuweka bayana taratibu za uteuzi wa viongozi wa Elimu katika ngazi za Shule, Kata, Halmashauri na Mikoa. Hivyo, malengo mahususi ya mwongozo huu ni pamoja na kubainisha sifa za uteuzi wa viongozi wa elimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekretarieti za Mikoa; kueleza taratibu za uteuzi wa viongozi hao na kubainisha hatua za kuchukuliwa na Mamlaka za Uteuzi wakati wa kutengua viongozi pale inapolazimu kufanya hivyo.

1.5 Matarajio

Inatarajiwa kuwa mwongozo huu utaweka taratibu ambazo zitawezesha upatikanaji wa viongozi bora katika elimu hivyo kuimarisha usimamizi na utoaji wa elimu bora.

1.6 Hitimisho

Sura hii imeonesha kwa muhtasari mamlaka ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI ya kuteua viongozi wa Elimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mikoa. Aidha, imefafanua umuhimu wa kuzingatia mwongozo wakati wa uteuzi wa viongozi pamoja na kuonesha watakaotumia mwongozo huu na matarajio yaliyopo.

SIFA ZA VIONGOZI WA ELIMU KATIKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA NA MIKOA

2.1 Utangulizi

Sura hii imebainisha sifa za viongozi wa elimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekretarieti za Mikoa. Sura imegawanyika katika sehemu kumi na moja (11) ambazo zimepangwa kulingana na nafasi ya kiongozi wa elimu kuanzia Shule, Kata, Halmashauri na Mikoa. Kada hizi za Uongozi zilizobainishwa katika ngazi mbalimbali kwenye sura hii ni pamoja na ngazi ya Shule (Mwalimu Mkuu/Mkuu wa Shule), ngazi ya Kata (Afisaelimu Kata), ngazi ya Halmashauri (Afisaelimu Taaluma Msingi/Sekondari, Afisaelimu Vifaa na Takwimu Msingi / Sekondari, Afisaelimu Elimu Maalum Msingi/ Sekondari, Afisaelimu wa Elimu ya Watu Wazima Msingi/ Sekondari na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi, Afisaelimu Msingi na Afisaelimu Sekondari) na ngazi ya Mkoa (Afisaelimu Taaluma Mkoa, Afisaelimu wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi Mkoa na Afisaelimu Mkoa) Mwisho hitimisho limetolewa.

2.2 Mwalimu Mkuu

Mwalimu Mkuu ni kiongozi Mkuu wa Shule ya Msingi. Uteuzi wa Mwalimu Mkuu hufanywa na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Ili kuweza kumteua Mwalimu Mkuu anatakiwa kuwa na sifa za kimuundo na kiutendaji kama ifuatavyo:

(a) Sifa za Kimuundo

Sifa za kimuundo za kuteuliwa kushika nafasi ya Mwalimu Mkuu ni kuwa na cheo cha muundo Mwalimu Mkuu IIB au Mwalimu Mkuu IB na awe na stashahada ya elimu na zaidi.

(b) Sifa za Kiutendaji

Sifa za kiutendaji za kuteuliwa kuwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi ni pamoja na:

i. Awe amefundisha katika Shule ya Msingi kwa kipindi kisichopungua miaka mitano (05);
ii. Awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai;
iii. Awe hajawahi kuvuliwa wadhifa wa Mkuu wa Shule kwa sababu zozote zile;
iv. Awe mwadilifu na mwenye mahusiano mazuri na jamii;
v. Awe na utendaji mzuri kulingana na Sera ya Menejimenti na

Ajira katika Utumishi wa Umma;
vi. Awe na uwezo wa kutumia MS Word, Excel, Power Point, Spread Sheets na intaneti;
vii. Awe na utendaji wa mafanikio wenye ushahidi katika majukumu aliyopewa kusimamia awali; na
viii. Awe mbunifu na mwenye uthubutu wa kutekeleza na kusimamia masuala ya elimu.

2.3 Mkuu wa Shule

Mkuu wa Shule ni kiongozi Mkuu wa Shule ya Sekondari. Uteuzi wa Mkuu wa Shule hufanywa na Katibu Tawala wa Mkoa. Ili kumteua Mkuu wa Shule anatakiwa kuwa na sifa za kimuundo na kiutendaji kama ifuatavyo:

(a) Sifa za Kimuundo

Sifa za kimuundo za kuteuliwa kushika nafasi ya Mkuu wa Shule ya Sekondari ni na cheo cha muundo cha Mwalimu Mkuu IIC au Mwalimu Mkuu IC na shahada ya elimu au zaidi.

(b) Sifa za Kiutendaji

Sifa za kiutendaji za kuteuliwa kuwa Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Serikali ni pamoja na:
i. Awe amefundisha katika Shule za Sekondari za Serikali kwa kipindi kisichopungua miaka mitano (05);
ii. Awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai;
iii. Awe hajawahi kuvuliwa wadhifa wa Mkuu wa Shule kwa sababu zozote zile;
iv. Awe mwadilifu na mwenye mahusiano mazuri na jamii;
v. Awe na utendaji mzuri kulingana na Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma;
vi. Awe na uwezo wa kutumia MS Word, Excel, Power Point, Spread Sheets na intanenti;
vii. Awe na utendaji wa mafanikio wenye ushahidi katika majukumu aliyopewa kusimamia awali; na
viii. Awe mbunifu na mwenye uthubutu wa kutekeleza na kusimamia masuala ya elimu.

2.4 Afisaelimu Kata

Uteuzi wa Afisaelimu Kata hufanywa na Katibu Tawala wa Mkoa. Ili kumteua Afisaelimu Kata anatakiwa kuwa na sifa za kimuundo na kiutendaji kama ifuatavyo:

(a) Sifa za Kimuundo

Sifa za kimuundo za kuteuliwa kushika nafasi ya kuwa Afisaelimu Kata ni kuwa na cheo cha muundo cha Mwalimu Mkuu IIC au Mwalimu Mkuu IC na kuwa na shahada ya elimu au zaidi.

(b) Sifa za Kiutendaji

Sifa za kiutendaji za kuteuliwa kuwa Afisaelimu Kata ni pamoja na:

i. Awe amekuwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi au Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Serikali kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu (03);
ii. Awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai;
iii. Awe hajawahi kuvuliwa wadhifa wa Mkuu wa Shule/Mwalimu Mkuu kwa sababu yoyote ile;
iv. Awe mwadilifu na mwenye mahusiano mazuri na jamii;
v. Awe na uwezo wa kutumia MS Word, Excel, Power Point, Spread Sheets na intanenti;
vi. Awe na utendaji wa mafanikio wenye ushahidi katika majukumu aliyopewa kusimamia awali; na
vii. Awe mbunifu na mwenye uthubutu wa kutekeleza na kusimamia masuala ya elimu.

2.5 Afisaelimu Taaluma Msingi/Sekondari

Uteuzi wa Afisaelimu Taaluma Msingi/ Sekondari hufanywa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Ili kumteua Afisaelimu Taaluma Msingi/Afisaelimu Taaluma Sekondari anatakiwa kuwa na sifa za kimuundo na kiutendaji kama ifuatavyo:

(a) Sifa za Kimuundo

Sifa za kimuundo za kuteuliwa kushika nafasi ya kuwa Afisaelimu Taaluma ni kuwa na cheo cha muundo cha Mwalimu Mkuu IIC au Mwalimu Mkuu IC na shahada ya elimu au zaidi.

(b) Sifa za Kiutendaji

Sifa za kiutendaji za kuteuliwa kuwa Afisa Taaluma Msingi/Sekondari ni pamoja na:

i. Awe amekuwa Afisaelimu Kata kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu (03);
ii. Awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai;
iii. Awe hajawahi kuvuliwa wadhifa wa Mkuu wa Shule/Mwalimu Mkuu au Afisaelimu Kata; kwa sababu yoyote ile;
iv. Awe mwadilifu na mwenye mahusiano mazuri na jamii;
v. Awe na utendaji mzuri kulingana na Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma;
vi. Awe na uwezo wa kutumia MS Word, Excel, Power Point, Spread Sheets na intanenti;

vii. Awe na utendaji wa mafanikio wenye ushahidi katika majukumu aliyopewa kusimamia awali; na
viii. Awe mbunifu na mwenye uthubutu wa kutekeleza na kusimamia masuala ya elimu.

2.6 Afisaelimu Vifaa na Takwimu Msingi / Sekondari wa Halmashauri

Uteuzi wa Afisaelimu Vifaa na Takwimu Msingi / Sekondari hufanywa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Ili kumteua Afisaelimu Vifaa na Takwimu Msingi/Sekondari anatakiwa kuwa na sifa za kimuundo na kiutendaji kama ifuatavyo:

(a) Sifa za Kimuundo

Sifa za kimuundo za kuteuliwa kushika nafasi ya kuwa Afisaelimu Vifaa na Takwimu ni kuwa na cheo cha muundo cha Mwalimu Mkuu IIC au Mwalimu Mkuu IC na shahada ya elimu au zaidi.

(b) Sifa za Kiutendaji

Sifa za kiutendaji za kuteuliwa kuwa Afisaelimu Vifaa na Takwimu Msingi/Sekondari ni pamoja na:

i. Awe amekuwa Afisaelimu Kata kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu (03);
ii. Awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai;
iii. Awe hajawahi kuvuliwa wadhifa wa Mkuu wa Shule/Mwalimu Mkuu na Afisaelimu Kata kwa sababu yoyote ile;
iv. Awe mwadilifu na mwenye mahusiano mazuri na jamii;
v. Awe na utendaji mzuri kulingana na Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma;
vi. Awe na uwezo wa kutumia MS Word, Excel, Power Point, Spread Sheets na intanenti;
vii. Awe na utendaji wa mafanikio wenye ushahidi katika majukumu aliyopewa kusimamia awali; na
viii. Awe mbunifu na mwenye uthubutu wa kutekeleza na kusimamia masuala ya elimu.

2.7 Afisaelimu wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi wa Halmashauri

Uteuzi wa Afisaelimu wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi hufanywa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Ili kumteua Afisaelimu wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi anatakiwa kuwa na sifa za kimuundo na kiutendaji kama ifuatavyo:

(a) Sifa za Kimuundo

Sifa za kimuundo za kuteuliwa kushika nafasi ya kuwa Afisaelimu wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi ni kuwa na cheo cha muundo cha Mwalimu Mkuu IIC au Mwalimu Mkuu IC na awe na Shahada ya Elimu ya Watu Wazima au zaidi.

(b) Sifa za Kiutendaji

Sifa za kiutendaji za kuteuliwa kuwa Afisaelimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi ni pamoja na:

i. Awe amekuwa Afisaelimu Kata kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu (03);
ii. Awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai;
iii. Awe hajawahi kuvuliwa wadhifa wa Afisaelimu Kata kwa sababu yoyote ile;
iv. Awe mwadilifu na mwenye mahusiano mazuri na jamii;
v. Awe na utendaji mzuri kulingana na Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma;
vi. Awe na utendaji wa mafanikio wenye ushahidi katika majukumu aliyopewa kusimamia awali;
vii. Awe na uwezo wa kutumia MS Word, Excel, Power Point, Spread Sheets na intanenti; na
viii. Awe mbunifu na mwenye uthubutu wa kutekeleza na kusimamia masuala ya elimu.

2.8 Afisaelimu Elimu Maalum Msingi/Sekondari

Uteuzi wa Afisaelimu Elimu Maalum hufanywa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Ili kumteua Afisaelimu Elimu Maalum anatakiwa kuwa na sifa za kimuundo na kiutendaji kama ifuatavyo:

(a) Sifa za Kimuundo

Sifa za kimuundo za kuteuliwa kushika nafasi ya kuwa Afisaelimu Elimu Maalum ni kuwa na cheo cha muundo cha Mwalimu Mkuu IIC au Mwalimu Mkuu IC na kuwa na Shahada ya elimu maalum au zaidi.

(b) Sifa za Kiutendaji

Sifa za kiutendaji za kuteuliwa kuwa Afisaelimu Elimu Maalumu ni pamoja na:

i. Awe amekuwa Afisaelimu Kata kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu (03);
ii. Awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai;
iii. Awe hajawahi kuvuliwa wadhifa wa Afisaelimu Kata kwa

sababu yoyote ile;
iv. Awe mwadilifu na mwenye mahusiano mazuri na jamii;
v. Awe na utendaji mzuri kulingana na Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma;
vi. Awe na uwezo wa kutumia MS Word, Excel, Power Point, Spread Sheets na intanenti;
vii. Awe na utendaji wa mafanikio wenye ushahidi katika majukumu aliyopewa kusimamia awali; na
viii. Awe mbunifu na mwenye uthubutu wa kutekeleza na kusimamia masuala ya elimu.

2.9 Afisaelimu wa Halmashauri Msingi/Sekondari

Uteuzi wa Afisaelimu wa Halmashauri Msingi/Sekondari hufanywa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Ili kumteua Afisaelimu wa Halmashauri Msingi/Sekondari anatakiwa kuwa na sifa za kimuundo na kiutendaji kama ifuatavyo:

(a) Sifa za Kimuundo

Sifa za kimuundo za kuteuliwa kuwa Afisaelimu wa Halmashauri ni kuwa na cheo cha muundo cha Mwalimu Mkuu IIC au Mwalimu Mkuu IC na kuwa na shahada ya uzamili au stashahada ya uzamili au zaidi.

(b) Sifa za Kiutendaji

Sifa za kiutendaji za kuteuliwa kuwa Afisaelimu wa Halmashuri ni pamoja na:

i. Awe Afisaelimu Taaluma Mkoa/Afisaelimu Maalum/Afisaelimu wa Elimu ya Watu Wazima/Elimu Nje ya Mfumo Rasmi Mkoa/ Afisaelimu Taaluma wa Halmashauri/Afisaelimu Vifaa na Takwimu/Afisaelimu Maalumu/Afisaelimu wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi au kuhudumu katika madaraka/cheo kinacholingana na vyeo hivyo;
ii. Awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai;
iii. Awe hajawahi kuvuliwa wadhifa wa vyeo tajwa hapo juu kwa sababu yoyote ile;
iv. Awe mwadilifu na mwenye mahusiano mazuri na jamii;
v. Awe na utendaji mzuri kulingana na Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma;
vi. Awe na uwezo wa kutumia MS Word, Excel, Power Point, Spread Sheets na intanenti;
vii. Awe na utendaji wa mafanikio wenye ushahidi katika majukumu aliyopewa kusimamia awali; na
viii. Awe mbunifu na uthubutu wa kutekeleza na kusimamia masuala ya elimu.

2.10 Afisaelimu Taaluma Mkoa

Uteuzi wa Afisaelimu Taaluma Mkoa hufanywa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Ili kumteua Afisaelimu Taaluma Mkoa anatakiwa kuwa na sifa za kimuundo na kiutendaji kama ifuatavyo:

(a) Sifa za Kumuundo

Sifa za kimuundo za kuteuliwa kushika nafasi ya kuwa Afisaelimu Taaluma Mkoa ni kuwa na cheo cha muundo cha Mwalimu Mkuu IIC au Mwalimu Mkuu IC na shahada ya elimu au zaidi.

(b) Sifa za Kiutendaji

Sifa za kiutendaji za kuteuliwa kuwa Afisaelimu Taaluma Mkoa ni pamoja na:

i. Awe ameshika vyeo vya Ngazi ya Halmashauri vya Afisaelimu Taaluma, Afisaelimu Vifaa na Takwimu, Afisaelimu wa Elimu ya Watu Wazima Na Afisaelimu Elimu Maalum kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu (03);
ii. Awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai;
iii. Awe hajawahi kuvuliwa wadhifa tajwa hapo juu kwa sababu yoyote ile;
iv. Awe mwadilifu na mwenye mahusiano mazuri na jamii;
v. Awe na utendaji mzuri kulingana na Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma;
vi. Awe na uwezo wa kutumia MS Word, Excel, Power Point, Spread Sheets na intanenti;
vii. Awe na utendaji wa mafanikio wenye ushahidi katika majukumu aliyopewa kusimamia; na
viii. Awe mbunifu na mwenye uthubutu wa kutekeleza na kusimamia masuala ya elimu.

2.11 Afisaelimu wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi Mkoa

Uteuzi wa Afisaelimu wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi Mkoa hufanywa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Ili kumteua Afisaelimu wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi anatakiwa kuwa na sifa za kimuundo na kiutendaji kama ifuatavyo:

(a) Sifa za Kimuundo

Sifa za kimuundo za kuteuliwa kushika nafasi ya kuwa Afisaelimu wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi ni kuwa na cheo cha muundo cha Mwalimu Mkuu IIC au Mwalimu Mkuu IC

na shahada ya elimu ya watu wazima au zaidi.

(b) Sifa za Kiutendaji

Sifa za kiutendaji za kuteuliwa kuwa Afisaelimu wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi Mkoa ni pamoja na:

i. Awe amekuwa Afisaelimu wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi katika Halmashauri kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu (03);
ii. Awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai;
iii. Awe hajawahi kuvuliwa wadhifa wa Afisaelimu wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi wa Halmashauri;
iv. Awe mwadilifu na mwenye mahusiano mazuri na jamii;
v. Awe na utendaji mzuri kulingana na Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma;
vi. Awe na uwezo wa kutumia MS Word, Excel, Power Point, Spread Sheets na intanenti;
vii. Awe na utendaji wa mafanikio wenye ushahidi katika majukumu aliyopewa kusimamia awali; na
viii. Awe mbunifu na mwenye uthubutu wa kutekeleza na kusimamia masuala ya elimu.

2. 12 Afisaelimu wa Mkoa

Uteuzi wa Afisaelimu wa Mkoa hufanywa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Ili kumteua Afisaelimu wa Mkoa anatakiwa kuwa na sifa za kimuundo na kiutendaji kama ifuatavyo:

(a) Sifa za Kimuundo

Sifa za kimuundo za kuteuliwa kushika nafasi ya kuwa Afisaelimu Mkoa ni kuwa na cheo cha muundo cha Mwalimu Mkuu IIC au Mwalimu Mkuu IC na kuwa na shahada ya uzamili au stashahada ya uzamili au zaidi.

(b) Sifa za Kiutendaji

Sifa za kiutendaji za kuteuliwa kuwa Afisaelimu wa Mkoa ni pamoja na:

i. Awe amekuwa Afisaelimu Halmashauri Msingi/Sekondari kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu (03) au kuhudumu katika madaraka/cheo kinacholingana na cheo cha Afisaelimu Halmashauri;
ii. Awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai;
iii. Awe hajawahi kuvuliwa wadhifa wa Afisaelimu Halmashauri kwa sababu yoyote ile;
iv. Awe mwadilifu na mwenye mahusiano mazuri na jamii;

v. Awe na utendaji mzuri kulingana na Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma;
vi. Awe na uwezo wa kutumia MS Word, Excel, Power Point, Spread Sheets na intanenti;
vii. Awe na utendaji wa mafanikio wenye ushahidi katika majukumu aliyopewa kusimamia awali; na
viii. Awe mbunifu na mwenye uthubutu wa kutekeleza na kusimamia masuala ya elimu.

2.13 Hitimisho

Sura hii imebainisha sifa za kimuundo na kiutendaji za mwalimu kuteuliwa kuwa kiongozi wa Elimumsingi na Sekondari katika ngazi ya Shule, Kata, Halmashauri na Mkoa. Pamoja na sifa nyingine za kimuundo na kiutendaji, sifa ya utendaji wa mafanikio wenye ushahidi katika majukumu aliyopewa kusimamia hapo awali iwe ndiyo msingi mkuu ili kupata viongozi bora wa Elimumsingi na Sekondari.

UTARATIBU WA UTEUZI WA VIONGOZI WA ELIMU KATIKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA NA MIKOA

3.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza uratatibu wa uteuzi wa viongozi wa elimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mikoa. Sura imegawanyika katika sehemu nane (08) ambazo zinahusiana na mchakato wa uteuzi wa Mwalimu Mkuu, Mkuu wa Shule, Afisaelimu Kata, Afisaelimu Msingi/ Sekondari wa Halmashauri, Afisaelimu Taaluma, Afisaelimu Vifaa na Takwimu, Afisaelimu Elimu Maalum Afisaelimu Elimu ya Watu Wazima na Nje ya Mfumo Rasmi wa Halmashauri, Afisaelimu Mkoa, Uteuzi wa Afisaelimu Taaluma Mkoa na na Uteuzi wa Afisaelimu Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi wa Mkoa. Mwisho, hitimisho limetolewa.

3. 2 Uteuzi wa Mwalimu Mkuu

Kwa minajili ya kufanya uteuzi wa Mwalimu Mkuu, Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi, Mchakato wa Mapendekezo ya Uteuzi pamoja na Mamlaka ya Uteuzi kufikia maamuzi zimebainishwa.

3.2.1 Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi

Kabla ya Mkurugenzi wa MSM hajamteua Mwalimu Mkuu anapaswa kuzingatia maoni ya Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi wa Mwalimu Mkuu. Kamati hiyo ina wajumbe watano ambao ni:

i. Afisaelimu Msingi au anayekaimu kwa barua ya Mkurugenzi wa Halmashauri au ya juu yake (Mwenyekiti);
ii. Afisaelimu Taaluma (Katibu),
iii. Katibu Msaidizi wa TSC (W) (Mjumbe); na
iv. Mthibiti Ubora Mkuu wa Shule (H) (Mjumbe).

3.2. 2 Mchakato wa Mapendekezo ya Uteuzi

Afisaelimu Msingi Halmashauri kwa kushirikiana na wasaidizi wake watakusanya majina na wasifu wa walimu ambao wanaonekana kuwa na uwezo wa kushika wadhifa wa Mwalimu Mkuu. Orodha hiyo itakusanywa kutoka kwa Walimu Wakuu au Maafisaelimu Kata au kwa njia ambayo wataona inafaa. Majina hayo yatajadiliwa na kikao cha Menejimenti ya Idara ya Elimu ya Msingi, Kikao cha Menejimenti ya idara kitapitisha majina yasiyopungua matatu kwa kila nafasi iliyo wazi na kuyawasilisha kwa Mkurugenzi wa Halmashauri pamoja na muhtasari wa kikao. Mkurugenzi akiridhia,

majina hayo yatawasilishwa kwa mamlaka za upekuzi. Baada ya upekuzi, Mkurugenzi wa Halmashauri atawasilisha majina yaliyorejeshwa kwenye Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi kwa ajili ya kujadiliwa. Muhtasari wa kikao cha Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi na majina yatawasilishwa kwa Mkurugenzi wa Halmshauri kwa hatua za uteuzi. Ushiriki wa kikao cha kamati ya mapendekezo ni wa lazima kwa wajumbe wote na Mwenyekiti atakuwa na kura ya turufu endapo kura za wajumbe za mapendekezo zitalingana, na hapaswi kuwakilishwa.

3.2.3 Mamlaka ya Uteuzi

Uteuzi wa Mwalimu Mkuu utafanywa na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kuzingatia majina yaliyowasilishwa na Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi.

3.3 Uteuzi wa Mkuu wa Shule

Kwa minajili ya kufanya uteuzi wa Mkuu wa Shule, Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi, Mchakato wa Mapendekezo ya Uteuzi pamoja na mamlaka ya uteuzi kufikia maamuzi zimebainishwa.

3.3.1 Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi

Uteuzi wa Mkuu wa Shule ya Sekondari hufanywa na Katibu Tawala wa Mkoa ambapo kabla hajamteua Mkuu wa Shule atazingatia maoni ya Kamati ya Mkoa ya Mapendekezo ya Uteuzi wa Mkuu wa Shule. Kamati hiyo ina wajumbe wafuatao:

i. Afisaelimu wa Mkoa au anayekaimu kwa barua ya Katibu Tawala wa Mkoa au barua ya wa juu yake (Mwenyekiti);
ii. Afisaelimu Taaluma wa Mkoa (Katibu); na
iii. Afisaelimu wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi wa Mkoa (Mjumbe).

Aidha kabla ya Mkurugenzi kupeleka majina Mkoani azingatie orodha ya majina yaliyowasilishwa na Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi wa Mkuu wa Shule ya Halmashauri ambayo ni;-

i. Afisaelimu Sekondari wa Halmashauri au anayekaimu kwa barua ya Mkurugenzi wa Halmashauri au barua ya wa juu yake (Mwenyekiti);
ii. Afisaelimu Taaluma Sekondari wa Halmashauri (Katibu);
iii. Katibu Msaidizi wa TSC (W) (Mjumbe);
iv. Mthibiti Ubora Mkuu wa Shule (H) (Mjumbe);

3.3.2 Mchakato wa Mapendekezo ya Uteuzi

Afisaelimu Sekondari Halmashauri kwa kushirikiana na wasaidizi wake watakusanya majina na wasifu wa walimu ambao wanaonekana kuwa na uwezo wa kushika wadhifa wa Mkuu wa Shule. Orodha hiyo itakusanywa kutoka kwa Wakuu wa Shule au Maafisaelimu Kata au kwa njia ambayo wataona inafaa.

Majina hayo yatajadiliwa na kikao cha Menejimenti ya Idara ya Elimu ya Sekondari na kisha kuwasilisha majina yasiyopungua matatu kwa kila nafasi iliyo wazi pamoja na muhtasari wa kikao kwa Mkurugenzi wa Halmashauri. Mkurugenzi akiridhia, majina hayo yatawasilishwa kwa mamlaka za upekuzi. Baada ya upekuzi, Mkurugenzi wa Halmashauri atawasilisha majina yaliorejeshwa kwenye Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi kwa ajili ya kujadiliwa. Kamati ya mapendekezo ya uteuzi wa Mkuu wa Shule ikikamilisha kazi yake itawasilisha muhtasari na majina kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ambaye atawasilisha majina hayo na muhtasari kwa Katibu Tawala Mkoa. Katibu Tawala Mkoa naye ataipatia Kamati ya Mkoa ya Mapendekezo ya Uteuzi wa Mkuu wa Shule. Kamati ya mapendekezo ya uteuzi wa Mkuu wa Shule ya Mkoa ikishakamilisha kazi itawasilisha muhtasari na majina kwa Katibu Tawala Mkoa ili ateue Wakuu wa Shule kulingana na nafasi zilizopo.

Ushiriki wa kikao cha Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi ni wa lazima. Nafasi ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi haina uwakilishi na ana kura ya turufu. endapo kura za wajumbe wa Kamati ya Uteuzi zitalingana.

3.3.3 Mamlaka ya Uteuzi

Uteuzi wa Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Serikali utafanywa na Katibu Tawala wa Mkoa kwa kuzingatia maelekezo ya Kamati ya Uteuzi.

3. 4 Uteuzi wa Afisaelimu Kata

Kwa minajili ya kufanya uteuzi wa Afisaelimu Kata, Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi, Mchakato wa Mapendekezo ya Uteuzi pamoja na mamlaka ya uteuzi kufikia maamuzi zimebainishwa.

3.4.1 Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi

Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi ya Afisaelimu Kata ya Halmashauri ina wajumbe watano ambao ni:

i. Afisaelimu Sekondari Halmashauri au anayekaimu kwa barua ya Mkurugenzi wa Halmashauri au barua ya wa juu yake

(Mwenyekiti);
ii. Afisaelimu Taaluma Msingi (Katibu);
iii. Afisaelimu Msingi Halmashauri (Mjumbe);
iv. Mthibiti Ubora Mkuu wa Shule (W) (Mjumbe); na
v. Katibu Msaidizi wa TSC (W) (Mjumbe).

3.4.2 Mchakato wa Mapendekezo ya Uteuzi

Afisaelimu Msingi na Sekondari Halmashauri kwa kushirikiana na wasaidizi wao watakusanya majina na wasifu wa Walimu Wakuu au Wakuu wa Shule ambao wanaonekana kuwa na uwezo wa kushika wadhifa wa Afisaelimu Kata. Orodha hiyo itakusanywa kutoka kwa Maafisaelimu Kata au kwa njia ambayo wataona inafaa. Majina hayo yatajadiliwa na Menejimenti ya Afisaelimu Msingi na Sekondari ambayo Mwenyekiti wa kikao cha menejimenti ya Elimu ya Msingi na Sekondari ni Afisaelimu Msingi na Katibu wake ni Afisaelimu Taaluma Sekondari. Muhtasari wa kikao hicho utawasilishwa na Mwenyekiti kwa Mkurugenzi wa Halmashauri.

Mkurugenzi akiridhia Majina hayo yatapelekwa kwa Mamlaka ya Upekuzi. Upekuzi ukikamilika Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri atawapatia Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi wa Afisaelimu Kata ya Halmashauri kwa ajili ya kujadiliwa. Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi wa Wakuu wa Shule ikikamilisha kazi yao watarejesha kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ambaye atawasilisha kwa Katibu Tawala Mkoa yakiwa na Muhtasari wa Maamuzi ya Kikao cha Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi.

Katibu Tawala wa Mkoa ataipatia Kamati ya mapendekezo uteuzi wa Afisaelimu Kata ya Mkoa ili wayajadili.Kamati ikishakamilisha kazi itamrejeshea Katibu Tawala wa Mkoa ili ateue Afisaelimu Kata kulingana na nafasi zilizopo kwa kuzingatia maoni ya kamati ya uteuzi ya mkoa yenye wajumbe wafuatao:
i. Afisaelimu Mkoa au anayekaimu kwa barua ya Katibu Tawala Mkoa au barua ya aliye juu yake (Mwenyekiti)
ii. Afisaelimu Taaluma Mkoa (Katibu)
iii. Afisaelimu wa Elimu ya Watu Wazima Mkoa

Ushiriki wa kikao cha Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi ni wa lazima. Nafasi ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi haina uwakilishi na ana kura ya turufu endapo kura za maamuzi ya wajumbe wa Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi zitalingana.

3.4.3 Mamlaka ya Uteuzi

Uteuzi wa Afisaelimu Kata utafanywa na Katibu Tawala wa Mkoa kwa kuzingatia majina yaliyopendekezwa na Kamati ya Uteuzi.

3.5 Uteuzi wa Afisaelimu Msingi/Sekondari wa Halmashauri

Kwa minajili ya kufanya uteuzi wa Afisaelimu Msingi na Afisaelimu Sekondari wa Halmashauri Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi, Mchakato wa Mapendekezo ya Uteuzi pamoja na Mamlaka ya Uteuzi kufikia maamuzi zimebainishwa.

3. 5.1 Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi

Afisaelimu Msingi/Sekondari wa MSM huteuliwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Kabla ya Katibu Mkuu hajamteua Afisaelimu MSM anapaswa kuzingatia maoni ya Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi wa Afisaelimu wa MSM. Kamati hiyo ina wajumbe watano ambao ni:

i. Naibu Katibu Mkuu (Elimu) - (Mwenyekiti);
ii. Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Elimu - (Katibu);
iii. Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu ya Sekondari - (Mjumbe);
iv. Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu ya Awali na Msingi - (Mjumbe); na
v. Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu Maalum, Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi - (Mjumbe).

3.5.2 Mchakato wa Mapendekezo ya Uteuzi

Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi itakuwa katika Ofisi ya Rais – TAMISEMI kama ilivyoainishwa hapo juu. Nafasi yoyote iliyoachwa wazi inapaswa kujazwa ndani ya miezi sita. Kamati ya Uteuzi itayajadili majina yaliyopendekezwa na Katibu Tawala wa Mkoa baada ya kushauriana na Afisaelimu Mkoa au kwa namna ambavyo mwenyekiti wa kamati hii atakavyoona inafaa.

Majina yatakayopendekezwa na Kamati ya Uteuzi yatawasilishwa kwa Katibu Mkuu kwa ajili ya hatua yake ya Uteuzi. Wateuliwa wote wa nafasi hizi za uongozi watalazimika kufanyiwa Upekuzi. Aidha, watathibitishwa kushika nyadhifa zao endapo taarifa za upekuzi kutoka kwenye mamlaka ya upekuzi zitaonesha kuwa wanayo maadili ya kutumikia katika nyadhifa hizo, na endapo taarifa za upekuzi za mteuliwa zitaonesha uwepo wa dosari yeyote, mteuliwa hatathibitishwa kwenye wadhifa wake, na ataondolewa.

3.5.3 Mamlaka ya Uteuzi

Uteuzi wa Afisaelimu wa Halmashauri hufanywa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kuzingatia mapendekezo ya Kamati ya Uteuzi.

3.6 Uteuzi wa Afisaelimu Taaluma, Afisaelimu Vifaa na Takwimu, Afisaelimu Elimu Maalum na Afisaelimu Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi wa Halmashauri

Kwa minajili ya kufanya uteuzi wa Afisaelimu Taaluma, Afisaelimu Vifaa na Takwimu, Afisaelimu Elimu Maalum na Afisaelimu Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi wa Halmashauri Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi, Mchakato wa Mapendekezo ya Uteuzi pamoja na mamlaka ya uteuzi kufikia maamuzi zimebainishwa.

3. 6.1 Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi

Afisaelimu Taaluma, Afisaelimu Vifaa na Takwimu, Afisaelimu Elimu Maalumu, na Afisaelimu Elimu ya Watu Wazima na Nje ya Mfumo Rasmi wa MSM huteuliwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Kabla ya Katibu Mkuu hajawateua viongozi hao anapaswa kuzingatia maoni ya Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi wa viongozi hao. Kamati hiyo itakuwa na wajumbe watano ambao ni:

i. Naibu Katibu Mkuu (Elimu) - (Mwenyekiti);
ii. Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Elimu - (Katibu);
iii. Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu ya Sekondari - (Mjumbe);
iv. Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu ya Awali na Msingi - (Mjumbe); na
v. Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu Maalum, Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi - (Mjumbe).

3.6.2 Mchakato wa Mapendekezo

Kamati ya mapendekezo ya uteuzi itakuwa katika Ofisi ya Rais – TAMISEMI kama ilivyoainishwa hapo juu. Nafasi yoyote iliyoachwa wazi inapaswa kujazwa ndani ya miezi sita. Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi itapokea na kuyajadili majina yaliyowasilishwa na Katibu Tawala wa Mkoa baada ya kushauriana na Afisaelimu Mkoa au kwa namna ambavyo mwenyekiti wa kamati hii atakavyoona inafaa.

Majina yatakayopendekezwa na Kamati ya Uteuzi yatawasilishwa kwa Katibu Mkuu kwa ajili ya hatua yake ya Uteuzi. Wateuliwa wote wa nafasi hizi za uongozi watalazimika kufanyiwa Upekuzi. Aidha, watathibitishwa kushika nyadhifa zao endapo taarifa za upekuzi kutoka kwenye mamlaka ya upekuzi zitaonesha kuwa wanayo

maadili ya kutumikia katika nyadhifa hizo, na endapo taarifa za upekuzi za mteuliwa zitaonesha uwepo wa dosari yeyote, mteuliwa hatathibitishwa kwenye wadhifa wake, na ataondolewa.

3.6.3 Mamlaka ya Uteuzi

Uteuzi wa wasaidizi wa Afisaelimu wa Halmashauri hufanywa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kuzingatia mapendekezo ya Kamati ya Uteuzi.

3.7 Uteuzi wa Afisaelimu Taaluma Mkoa/Afisaelimu Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi wa Mkoa

Kwa minajili ya kufanya uteuzi wa Uteuzi wa Afisaelimu Taaluma Mkoa/Afisaelimu Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi wa Mkoa, Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi, Mchakato wa Mapendekezo ya Uteuzi pamoja na Mamlaka ya Uteuzi kufikia maamuzi zimebainishwa.

3.7.1 Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi

Afisaelimu Taaluma na Afisaelimu Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi wa Mkoa huteuliwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Kabla ya Katibu Mkuu hajawateua viongozi hao anapaswa kuzingatia maoni ya Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi wa viongozi hao. Kamati hiyo ina wajumbe watano ambao ni:

i. Naibu Katibu Mkuu (Elimu) - (Mwenyekiti);
ii. Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Elimu - (Katibu);
iii. Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu ya Sekondari - (Mjumbe);
iv. Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu ya Awali na Msingi - (Mjumbe); na
v. Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu Maalum, Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi - (Mjumbe).

3.7.2 Mchakato wa Mapendekezo ya Uteuzi

Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi itakuwa katika Ofisi ya Rais – TAMISEMI kama ilivyoainishwa hapo juu. Nafasi yoyote iliyoachwa wazi inapaswa kujazwa ndani ya miezi sita. Kamati ya Uteuzi itapokea na kujadili majina yanayopendekezwa na Katibu Tawala wa Mkoa baada ya kushauriana na Afisaelimu Mkoa au kwa namna ambavyo mwenyekiti wa kamati hii atakavyoona inafaa.

Majina yatakayopendekezwa yatawasilishwa kwa Katibu Mkuu kwa ajili ya hatua yake ya Uteuzi. Wateuliwa wote wa nafasi hizi za uongozi

watalazimika kufanyiwa Upekuzi. Aidha, watathibitishwa kushika nyadhifa zao endapo taarifa za upekuzi kutoka kwenye mamlaka ya upekuzi zitaonesha kuwa wanayo maadili ya kutumikia katika nyadhifa hizo, na endapo taarifa za upekuzi za mteuliwa zitaonesha uwepo wa dosari yeyote, mteuliwa hatathibitishwa kwenye wadhifa wake, na ataondolewa.

3.7.3 Mamlaka ya Uteuzi

Uteuzi wa Afisaelimu Taaluma na Afisaelimu Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi utafanywa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kuzingatia mapendekezo ya Kamati ya Uteuzi.

3.8 Uteuzi wa Afisaelimu wa Mkoa

Kwa minajili ya kufanya uteuzi wa Uteuzi wa Afisaelimu wa Mkoa, Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi, Mchakato wa Mapendekezo ya Uteuzi pamoja na mamlaka ya uteuzi kufikia maamuzi zimebainishwa.

3.8.1 Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi

Afisaelimu wa Mkoa huteuliwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Kabla ya Katibu Mkuu hajamteua Afisaelimu wa Mkoa anapaswa kuzingatia maoni ya kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi wa Afisaelimu wa Mkoa. Kamati hiyo itakuwa na wajumbe watano ambao ni:

i. Naibu Katibu Mkuu (Elimu) - (Mwenyekiti);
ii. Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Elimu - (Katibu);
iii. Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu ya Sekondari - (Mjumbe);
iv. Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu ya Awali na Msingi - (Mjumbe); na
v. Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu Maalum, Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi - (Mjumbe).

3.8.2 Mchakato wa Mapendekezo ya Uteuzi

Kamati ya mapendekezo ya uteuzi itakuwa katika Ofisi ya Rais – TAMISEMI kama ilivyoainishwa hapo juu. Nafasi yoyote iliyoachwa wazi inapaswa kujazwa ndani ya miezi sita. Kamati ya Uteuzi itapokea na kuyajadili majina yaliyopendekezwa na Katibu Tawala wa Mkoa baada ya kushauriana na Afisaelimu Mkoa au kwa namna ambavyo mwenyekiti wa kamati hii atakavyoona inafaa.

Majina yatakayopendekezwa na Kamati ya Uteuzi yatawasilishwa kwa Katibu Mkuu kwa ajili ya hatua yake ya Uteuzi. Wateuliwa wote

wa nafasi hizi za uongozi watalazimika kufanyiwa Upekuzi. Aidha, watathibitishwa kushika nyadhifa zao endapo taarifa za upekuzi kutoka kwenye mamlaka ya upekuzi zitaonesha kuwa wanayo maadili ya kutumikia katika nyadhifa hizo, na endapo taarifa za upekuzi za mteuliwa zitaonesha uwepo wa dosari yeyote, mteuliwa hatathibitishwa kwenye wadhifa wake, na ataondolewa.

3.8.3 Mamlaka ya Uteuzi

Baada ya taratibu za uteuzi kukamilika, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – TAMISEMI atafanya uteuzi wa Afisaelimu wa Mkoa kwa kuzingatia mapendekezo ya Kamati ya Uteuzi.

3.9 Utaratibu wa Kutengua Viongozi wa Elimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mikoa

Mamlaka ya uteuzi ndio mamlaka ya kutengua. Mamlaka itauanda timu ya uchunguzi ambayo itatoa ushauri. Hata hivyo, timu ya uchunguzi itapaswa kumpatia haki ya kusikilizwa kiongozi wa elimu katika ngazi husika kabla ya kuchukua maamuzi.

Kiongozi yeyote wa Elimumsingi na Sekondari ataondolewa kwenye nafasi yake endapo atashindwa kutekeleza ipasavyo majukumu yake au endapo sifa za kiutendaji alizoonesha kabla ya kuteuliwa kuondoka, au taarifa za upekuzi kuonesha amekuwa na dosari za kiuadilifu.

3. 10 Hitimisho

Sura hii imebainisha taratibu zinapaswa kufuatwa wakati wa kuteua au kutengua wa viongozi wa Elimumsingi na Sekondari. Mchakato na Mamlaka za Uteuzi zimewekwa wazi. Ni jukumu la Mamlaka kuzingatia mchakato huo ili kupata viongozi bora kwenye ngazi za Uongozi wa Elimumsingi na Sekondari za Shule, Kata, Halmashauri na Mikoa. Itakuwa ni wajibu wa kila aliyepewa dhamana ya kufanya uteuzi wa viongozi wa elimu katika ngazi mbalimbali kutekeleza wajibu wake kwa kuzingatia Mwongozo huu.

SURA YA NNE

KANUNI ZA UENDESHAJI WA KAMATI ZA MAPENDEKEZO YA UTEUZI WA VIONGOZI WA ELIMU KATIKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA NA MIKOA

4. 1 Utangulizi

Sura hii inaeleza kwa muhtasari kanuni za kuzingatia wakati wa kuteua viongozi. Lengo la kubainisha kanuni hizi ni kuweka misingi ya uwazi na uadilifu wakati wa kusimamia uteuzi wa viongozi wa elimu katika ngazi za Shule, Kata, Halmashauri na Mikoa.

4. 2 Kanuni za Uendeshaji wa Kamati za Uteuzi

Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi wa viongozi wa ngazi mbalimbali itazingatia kanuni zifuatazo:

i. Kutokufanya ubaguzi wa aina yoyote ile wakati wa utekelezaji wa majukumu yao kwa misingi ya kabila, jinsia, ukanda na dini;
ii. Kuzingatia haki za binadamu;
iii. Kuwa waadilifu katika utekelezaji wa majukumu yao;
iv. Kutunza siri;
v. Kufanya kazi kwa weledi;
vi. Kuwepo kwa uwazi na ukweli;
vii. Nafasi ya mwenyekiti haina uwakilishi;
viii. Mwenyekiti wa kamati atakuwa na kura turufu pale tu kura za awali zitakapokuwa sawa;
ix. Kila kikao lazima kiandaliwe Muhtasari utakaotunzwa na kuwasilishwa kwa ngazi ya juu kwa hatua zaidi; na
x. Kamati hizi kufuata sera, sheria, kanuni zilizopo na maelekezo ya Serikali kupitia Nyaraka mbalimbali zilizopo na zitakazoendelea kutolewa.

4. 3 Hitimisho

Sura hii imeweka bayana Kanuni kumi (10) zinazopaswa kuzingatia wakati wa mchakato wa Kamati za Uteuzi wa viongozi wa elimu katika ngazi za Shule, Kata, Halmashauri na Mikoa. Hivyo, Kamati za Uteuzi wa viongozi zitapaswa kuzingatia kanuni hizo wakati wa utekelezaji wa majukumu yao.

MAJUMUISHO NA HITIMISHO

5.1 Utangulizi

Sura hii ina sehemu mbili (02) ambazo ni majumuisho na hitimisho. Majumuisho yanaelezea kwa muhtasari kuhusu yaliyowasilishwa katika sura ya kwanza hadi nne. Hitimisho linatoa mwelekeo wa utekelezaji wa mwongozo ili kufikia matarajio.

5.2 Majumuisho

Mwongozo wa Uteuzi wa Viongozi wa Elimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mikoa katika Elimumsingi na sekondari una sura tano. Sura ya kwanza imebainisha mamlaka ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI katika kuteua viongozi wa elimu katika ngazi za Shule, Kata, Halmashauri na Mikoa. Aidha, katika sura hiyo, usuli na mabadiliko mbalimbali yaliopitiwa katika usimamizi na uendeshaji wa Elimumsingi na Sekondari yamewekwa bayana.

Sura ya pili imebainisha sifa za kimuundo na kiutendaji za kuteuliwa kuwa kiongozi kwa ngazi zote kuanzia Mwalimu Mkuu hadi Afisaelimu wa Mkoa. Aidha, sura ya tatu inaeleza mchakato na taratibu za kuzingatia katika kufanya uteuzi wa viongozi wa elimu katika ngazi zote. Sehemu ya nne imejikita kujadili kanuni za kuzingatia wakati wa uteuzi wa viongozi wa Elimumsingi na Sekondari kwa muhtasari, na sura ya tano imehitimisha.

5.3 Hitimisho

Mwongozo huu unapaswa kutekelezwa kwa ufanisi ili kuwezesha upatikanaji wa viongozi bora wa elimu katika ngazi za Shule, Kata, Halmashauri na Mikoa. Ofisi ya Rais - TAMISEMI inaamini kuwa Mwongozo huu utaweka msingi imara wa upatikanaji wa viongozi wa elimu katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa unaozingatia weledi, ujuzi, uzoefu na ubunifu; na bila upendeleo, huba au kwa kujuana.



Mji wa Serikali - Mtumba
Mtaa wa TAMISEMI
S.L.P 1923, Dodoma
Simu : (255) 26 232 1 234
Barua Pepe : ps@tamisemi.go.tz

www.tamisemi.go.tz